



JAMHURI YA MUUNGANO  
WA TANZANIA



# ISTILAHI ZA KISHERIA



OFISI YA MWANASHERIA MKUU  
WA SERIKALI



## THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

### ISTILAHIZA KISHERIA



**Prepared by  
The Office of the  
Attorney General  
December, 2023**

**Copyright ©2023  
First Printing, 2023  
[www.agctz.go.tz](http://www.agctz.go.tz)**



Following directives of the Government in the year 2020 that Kiswahili should be the official language in the public legal sector, the Interpretation of Laws Act, Cap. 1, was subsequently amended through the Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No.1 of 2021. In response to this amendment, the Office of the Attorney General responsible for legislative drafting and translation of laws has taken deliberate efforts to ensure the implementation of the directives. This includes compiling a list of legal terminologies and related expressions to aid in translation between English and Kiswahili languages.

Therefore, this Publication contains a compilation of the legal terminologies commonly used in legislation and other documents, that have been translated from English to Kiswahili languages. The aim is to improve public understanding and participation in the legal system. The Publication seeks to address challenges encountered by the Office of the Attorney General and its stakeholders in legislative drafting, translation and revision of the laws.

More often than not, the challenges experienced are associated with lack of standard guidelines that set ground for translation of words and legal terminologies. This lack of standardization can result in multiple meanings for one word or terminology. This has caused confusion among stakeholders regarding the use and application of certain words or terminologies to the extent that it impairs implementation of legislation in accordance with spirit envisioned by the Parliament. In addition, similar challenges have been experienced in the preparation of legal instruments and other documents.

Kiswahili as the official language of the Nation and one that is widely spoken and easily understood by the public, holds a significant historical importance in our nation and plays a vital role in fostering awareness and encouraging community involvement in various legal processes and procedures. Thus, translation of the terminologies under this Publication has been executed with utmost skill and care, taking into account the accuracy of the intended meaning.

This Publication is introduced with the belief that it will facilitate equitable access to legal information and act as an indispensable tool, thereby contributing positively to sustainable development and administration of justice within our society.

We extend our best wishes to all readers in their endeavor to comprehend and appreciate this Publication.



**Hon. Judge Dr. Eliezer Mbuki Feleshi**  
**ATTORNEY GENERAL**  
**1<sup>st</sup> December, 2023.**

Kufuatia maagizo ya Serikali ya Mwaka 2020 kwamba Kiswahili kiwe lugha rasmi katika Tasnia ya Sheria, Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura 1, ilifanyiwa marekebisheso kuitia Sheria ya Marekebisheso ya Sheria Mbalimbali (Na.1) ya Mwaka 2021. Kutokana na marekebisheso hayo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuitia Divisheni ya Uandishi wa Sheria ambayo ndiyo yenye jukumu la kutafsiri sheria, imefanya kazi maelekezo hayo na kuanda Istilahi za Misamiati ya Kisheria na inayotumiwa mara kwa mara na Mawakili wa Serikali, hususan, Waandishi wa Sheria kwa ajili ya kurahisisha shughuli za Ufasiri wa Sheria kutoka lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili na kinyume chake.

Kwa hivyo, Chapisho hili lina istilahi za kisheria ambazo hutumika sana katika sheria na hati zingine ambazo zimetafsiriwa kutoka Kiingereza kwenda lugha ya Kiswahili. Madhumuni ni kuboresha uelewa wa umma na ushiriki katika mfumo wa sheria. Chapisho hili linalenga kukabiliana na changamoto zinazoikabili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wadau wake katika utungaji wa sheria, tafsiri na marekebisheso ya sheria.

Mara nyingi, kumemetokea changamoto za matumizi ya misamiati hiyo kutokana ukosefu wa miongozo sanifu inayoweka msingi wa tafsiri ya maneno na istilahi za kisheria, na hivyo kuwepo na uwezekano wa kuwa na maana zaidi ya moja kwa neno au istilahi moja katika matumizi ya muktadha mmoja. Hali hii imesababisha mkanganyiko mionganoni mwa Mawakili wa Serikali na wadau wengine kuhusu matumizi ya baadhi ya misamiati au istilahi jambo ambalo linaweza kudhoofisha utekelezaji wa sheria na kushindwa kufikia lengo la kutungwa kwa sheria husika. Aidha, changamoto kama hizo zimejitokeza katika utayarishaji wa hati na nyaraka nyingine za Serikali.

Kiswahili kama lugha rasmi ya Taifa inayozungumzwa na watu wengi na kueleweka kwa urahisi, ina umuhimu mkubwa katika historia ya Taifa letu na ina mchango mkubwa katika kukuza uelewa na kuhimiza ushiriki wa jamii katika michakato na mambo mbalimbali ya kisheria na kimaendeleo, kwa ujumla. Hivyo, tafsiri ya istilahi za misamiati ya kisheria kwa lugha ya Kiswahili imefanyaika kwa ustadi na umakini mkubwa kwa kuzingatia maana iliyokusudiwa na sheria husika.

Istilahi za Baadhi ya Misamiati ya Kisheria imeandaliwa kwa imani kwamba itasaidia upatikanaji rahisi na kutumika kama rasilimali yenyeye thamani, na hivyo kuchangia vyema katika utekelezaji wa shughuli za ki maendeleo na utawala wa haki ndani ya jamii zetu.

Tunawatachia kila la kheri wasomaji na watumiaji wa Chapisho hili katika shughuli zao za kila siku.



**Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi**  
**MAWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**  
**1 Disemba, 2023.**



From a technical standpoint, the translation of terminologies between English and Kiswahili languages invariably encountered in the legislative drafting and translation of laws processes is mainly associated with lack of standardised guidelines. These challenges have resulted to inconsistencies, ambiguities, substandard translation of words or terminologies used in legislation, as well as failure to translate words or terminologies within their appropriate context. In view of the above, this Publication aims to provide solutions for the challenges encountered by the Office of the Attorney General in the translation of legislation and other documents.

My sincere gratitude extends to the Hon. Attorney General, Judge Dr. Eliezer Mbuki Feleshi and the Chief Parliamentary Drafter, Mr. Onorius John Njole. In addition, I would also like to take this opportunity to express my sincere gratitude to Hon. Judge Dr. Evaristo Longopa, for his dedication and great support to me and the Legislative Drafting Division in the preparation of these terms. A special thanks to the National Kiswahili Council and the former Retired Chief Parliamentary Draftsman, Ms. Sarah Kinyamfura Barahomoka for their invaluable contribution to this project.

I would also wish to express my gratitude to the entire Management team of the Office of the Attorney General for their support in this project.

My heartfelt gratitude goes to the staff of the Legislative Drafting Division of the Office of Attorney General for their tireless efforts in preparing this List. It fills me with immense pride to recognize that the Legislative Drafting Division boasts a creative and hardworking workforce, which has been instrumental in the success of this exercise.

I wish all readers and users of this list an enjoyable and enlightening experience in their reading!

A handwritten signature in black ink, appearing to read "Hon. Amb. Prof. Kennedy G. Gastorn".

**Hon. Amb. Prof. Kennedy G. Gastorn**  
**1<sup>st</sup> December, 2023.**

Kwa mtazamo wa kitaalamu, changamoto katika matumizi ya istilahi za kisheria kutoka katika lugha ya Kiingereza kwenda katika lugha ya Kiswahili na kinyume chake ambazo mara kwa mara tumekumbana nazo katika michakato ya Uandishi na Ufasiri wa Sheria kwa kiasi kikubwa zinatokana na kukosekana kwa istilahi sahihi katika lugha ya Kiswahili. Hali hiyo imepelekeea kutokuwepo kwa uthabiti wa matumizi ya istilahi, kuibuka kwa utata wa tafsiri, ubora hafifu wa sheria zinazotafsiriwa na kushindwa kutafsiri misamiati na istilahi kwa kuzingatia muktadha sahihi.

Kutokana na changamoto hizo, Chapisho hili linakusudia kutatta changamoto hizo ambazo Ofisi ya Mwanasheria Mkoo wa Serikali imekuwa ikikumbana nazo katika Ufasiri wa Sheria na nyaraka nyinginezo.

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Mwanasheria Mkoo wa Serikali, Jaji Dkt. Eliezer Mbuki Feleshi na Mwandishi Mkoo wa Sheria, Bw. Onorius John Njole. Aidha, napenda pia kuchukua fursa hii, kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mhe. Jaji Dkt. Evaristo Longopa, kwa kujitolea na kutoa msaada mkubwa kwangu na kwa Divisheni ya Uandishi wa Sheria katika utayarishaji wa istilahi hizi. Shukurani za kipekee ziende kwa Baraza la Kiswahili Tanzania, Mwandishi Mkoo wa Sheria Mstaafu, Bi. Sarah Kinyamfura Barahomoka kwa mchango wao usiopimika.

Vilevile, shukrani zangu za dhati ziwaendee watumishi wa Divisheni ya Uandishi wa Sheria kwa juhudi zao za dhati katika kuandaa istilahi hizi. Inanipa fahari kubwa kutambua kwamba Divisheni ya Uandishi wa Sheria inao watumishi wabunifu na wachapakazi ambao wameweza kupelekeea zoezi hili kuwa lenye mafanikio.

Nawatakia kila la kheri wasomaji na watumiaji wa istilahi hizi.



**Mhe. Balozi Prof. Kennedy G. Gastorn**  
**NAIBU MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**  
**1 Disemba, 2023.**

## A

|     |   |  |
|-----|---|--|
| 1.  | <b><i>ab initio</i></b><br><b><i>"void ab initio"</i></b> | toka mwanzo<br>"batili toka mwanzo"                          |
| 2.  | <b>absolute</b>   | kamili/isyo na ukomo/ thabiti                                |
| 3.  | <b>accede</b>   | ridhia/kubali ( hususan baada ya washiriki wengine kuridhia) |
| 4.  | <b>accrue</b>   | ongezeka/zidi/ tokana na/ patikana                           |
| 5.  | <b>acquire</b>  | pata/twaa  |
| 6.  | <b>Act</b>  | Sheria   |
|     | <b>act</b>  | kitendo/ tenda   |
| 7.  | <b>act or omission</b>                                    | tenda au kutotenda   |
| 8.  | <b>action</b>   | kitendo/ hatua   |
| 9.  | <b>ad hoc</b>   | kusudi maalumu / dharura/ mahususi                           |
| 10. | <b>address</b>  | anwani/eleza   |
| 11. | <b>adjudicate</b>   | toa uamuzi/tekeleza taratibu za kufikia uamuzi               |
| 12. | <b>admissible</b>   | - enye kukubalika katika Mahakama au chombo cha kisheria     |
| 13. | <b>admit</b>  | kubali/ kiri   |
| 14. | <b>adopt</b>  | kubali/asili(mtoto)  |
| 15. | <b>affidavit</b>  | hatikiapo  |
| 16. | <b>Affix</b>  | bandika/weka/tia (saini)                                     |
| 17. | <b>afford a right</b>                                     | toa haki   |
| 18. | <b>age of majority</b>                                    | umri kuanzia miaka 18  |
| 19. | <b>age of minority</b>                                    | umri chini ya miaka 18                                       |
| 20. | <b>agreement</b>  | makubaliano/mapatano / maafikiano                            |
| 21. | <b>allege</b>   | dai/tuhumu   |
| 22. | <b>alter</b>  | badilisha  |
| 23. | <b>ambiguous</b>  | -enye utata/ -enye kutafsirika kwa maana zaidi ya moja       |
| 24. | <b>amend</b>  | badilisha/rekebisha  |
| 25. | <b>amicus curiae</b>                                      | Rafiki wa mahakama   |
| 26. | <b>among other things</b>                                 | miongoni mwa mambo/masuala                                   |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|     |                                |   |
|-----|--------------------------------|---|
|     |                                | mengine/ pamoja na mambo/ masuala mengine         |
| 27. | <b>annexure</b>                | kiambatisho                                       |
| 28. | <b>apparent</b>                | dhahiri/wazi                                      |
| 29. | <b>appeal</b>                  | rufaa/kata rufaa                                  |
| 30. | <b>appraise</b>                | tathmini/thamini                                  |
| 31. | <b>apprentice</b>              | mwanagenzi  |
| 32. | <b>apprise</b>                 | arifu / pasha habari                              |
| 33. | <b>appropriate</b>             | sahihi/ enye kustahili                            |
| 34. | <b>approve</b>                 | idhinisha   |
| 35. | <b>approved budget</b>         | bajeti iliyoidhinishwa                            |
| 36. | <b>approved Draft Bill</b>     | rasimu ya Muswada ulioidhinishwa                  |
| 37. | <b>approved school</b>         | shule ya maadilisho                               |
| 38. | <b>arbitrate/arbitration</b>   | suluhisha/usuluhishi                              |
| 39. | <b>arbitrator</b>              | mwamuzi/msuluhishi                                |
| 40. | <b>arising out of</b>          | inayotokana na                                    |
| 41. | <b>arrears</b>                 | malimbikizo                                       |
| 42. | <b>articles of association</b> | kanuni za kampuni                                 |
| 43. | <b>as the case may be</b>      | kadiri inavyoweza kuwa/ vyovyyote inavyoweza kuwa |
| 44. | <b>assent</b>                  | kubali/ridhia/ idhinisha                          |
| 45. | <b>attach</b>                  | ambatisha   |
| 46. | <b>Authority</b>               | Mamlaka   |
| 47. | <b>authority</b>               | mamlaka/ uwezo                                    |
| 48. | <b>award</b>                   | hukumu/ uamuzi/ tuzo                              |

## B

|     |  |                             |
|-----|--|-----------------------------|
| 49. | <b>beneficial owner</b>                        | mnufaika husika / wa mwisho |
| 50. | <b>bequeath</b>                                | rithisha                    |
| 51. | <b>body</b><br><b>corporate/corporate body</b> | chombo/ shirika hodhi       |
| 52. | <b>bona fide (good faith)</b>                  | nia njema                   |
| 53. | <b>by-law</b>                                  | sheria ndogo                |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|          |   |  |
|----------|---|--|
| 54.      | <b>by virtue of</b>                       | kwa sababu ya                                |
| <b>C</b> |   |  |
| 55.      | <b>cabinet</b>                            | baraza la mawaziri                           |
| 56.      | <b>casting vote</b>                       | kura ya maamuzi                              |
| 57.      | <b>cause of action</b>                    | sababu ya msingi wa madai                    |
| 58.      | <b>caveat</b>                             | pingamizi                                    |
| 59.      | <b>cease</b>                              | koma/isha/acha                               |
| 60.      | <b>certify</b>                            | thibitisha                                   |
| 61.      | <b>chapter</b>                            | Sura/ Sehemu                                 |
| 62.      | <b>charter</b>                            | mkataba/ hatiidhini                          |
| 63.      | <b>Chief Justice</b>                      | Jaji Mkuu                                    |
| 64.      | <b>citation</b>                           | jina   |
| 65.      | <b>cited as</b>                           | itajulikana kama/itafahamika<br>kama/itaitwa |
| 66.      | <b>civil procedure</b>                    | mwenendo wa madai                            |
| 67.      | <b>claim</b>                              | madai  |
| 68.      | <b>class</b>                              | daraja/ ngazi                                |
| 69.      | <b>classify/classified/classification</b> | ainisha/iliyoainishwa/uainishaji             |
| 70.      | <b>clerk/clerk</b>                        | karani/katibu                                |
| 71.      | <b>code</b>                               | sheria /kanuni                               |
| 72.      | <b>collateral</b>                         | dhamana                                      |
| 73.      | <b>come into force</b>                    | kuanza kutumika/uhalali                      |
| 74.      | <b>commencement</b>                       | kuanza kutumika                              |
| 75.      | <b>commissioner for oaths</b>             | kamishna wa viapo                            |
| 76.      | <b>common law</b>                         | sheria za mfumo wa Jumuiya ya Madola         |
| 77.      | <b>commonwealth countries</b>             | nchi za Jumuiya ya Madola                    |
| 78.      | <b>company</b>                            | kampuni                                      |
| 79.      | <b>compensation</b>                       | fidia  |
| 80.      | <b>competent</b>                          | -enye uwezo                                  |
| 81.      | <b>competent authority</b>                | mamlaka husika/yenye dhamana                 |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|      |                                |                                |
|------|--------------------------------|--------------------------------|
| 82.  | <b>comply/compliance</b>       | zingatia/uzingatiaji           |
| 83.  | <b>composition</b>             | muundo                         |
| 84.  | <b>compound</b>                | fifilisha                      |
| 85.  | <b>conceal</b>                 | ficha                          |
| 86.  | <b>concession</b>              | makubaliano                    |
| 87.  | <b>conciliate/conciliation</b> | patanisha/upatanishi           |
| 88.  | <b>condition</b>               | masharti                       |
| 89.  | <b>conduct</b>                 | endesha/ongoza/mwenendo        |
| 90.  | <b>confiscate</b>              | nyang'anya/ taifisha           |
| 91.  | <b>conflict of interest</b>    | mgongano wa kimaslahi          |
| 92.  | <b>conform/conformity</b>      | kubaliana/endana               |
| 93.  | <b>consensus</b>               | mwafaka/makubaliano/maridhiano |
| 94.  | <b>consent</b>                 | ridhaa/kubali/ idhini          |
| 95.  | <b>consequences</b>            | matokeo/madhara                |
| 96.  | <b>constitution</b>            | katiba/muundo                  |
| 97.  | <b>construe</b>                | tafsiri                        |
| 98.  | <b>contrary</b>                | kinyume na/kwa upande mwingine |
| 99.  | <b>contract</b>                | mkataba                        |
| 100. | <b>contradict</b>              | pingana na/hitilafiana/kinzana |
| 101. | <b>contravene</b>              | kiuka                          |
| 102. | <b>convene</b>                 | kutanisha/ itisha              |
| 103. | <b>convict</b>                 | tia hatiani                    |
| 104. | <b>co-opt</b>                  | shirikisha/ azima              |
| 105. | <b>court</b>                   | mahakama                       |
| 106. | <b>covenant</b>                | makubaliano/ mapatano          |
| 107. | <b>circular</b>                | waraka                         |
| 108. | <b>custody</b>                 | ulinzi/uangalizi/ kizuizi      |
| 109. | <b>custom</b>                  | mila/desturi                   |

## D

|      |                            |                  |
|------|----------------------------|------------------|
| 110. | <b>damage</b>              | haribu/uharibifu |
| 111. | <b>damages</b>             | fidia/ hasara    |
| 112. | <b>de novo</b>             | upya/ mwanzo     |
| 113. | <b>declare/declaration</b> | tamka/tamko      |
| 114. | <b>decree</b>              | amri             |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|      |                             |   |
|------|-----------------------------|---|
| 115. | <b>deed</b>                 | hati                                      |
| 116. | <b>Defraud</b>              | danganya/laghai.                          |
| 117. | <b>default</b>              | shindwa/ kutofanya                        |
| 118. | <b>delegate/delegation</b>  | kasimu/ukasimishaji( kimataifa-ujumbe)    |
| 119. | <b>delete</b>               | futa/ ondoa                               |
| 120. | <b>demand</b>               | hitaji/taka/dai                           |
| 121. | <b>denounce</b>             | kana/kanusha                              |
| 122. | <b>deny/denial</b>          | kana/kanusha/ kataa/nyima                 |
| 123. | <b>deposit</b>              | amana/weka fedha benki/ wasilisha nyaraka |
| 124. | <b>deprive</b>              | nyima, kosesha.                           |
| 125. | <b>derogate</b>             | punguza/nyima haki/ kukengeuka            |
| 126. | <b>detain/ detention</b>    | zuia/weka kizuizini/ kushikilia           |
| 127. | <b>determine</b>            | amua                                      |
| 128. | <b>discharge</b>            | tekeleza/achilia                          |
| 129. | <b>disclose</b>             | toa/fichua/weka wazi                      |
| 130. | <b>discretion</b>           | hiari/chaguo/utashi                       |
| 131. | <b>dismiss/dismissal</b>    | kataa/ tupa/ futa                         |
| 132. | <b>dispute</b>              | mgogoro/ ubishani/ pinga                  |
| 133. | <b>doctrine</b>             | kanuni                                    |
| 134. | <b>document</b>             | hati/waraka                               |
| 135. | <b>documentary evidence</b> | ushahidi wa nyaraka                       |
| 136. | <b>draft</b>                | rasimu                                    |
| 137. | <b>draftsman</b>            | msawidi/ mwandishi wa sheria              |
| 138. | <b>due</b>                  | kupasa/-enye kustahili                    |
| 139. | <b>duly</b>                 | Ipasavyo / -enye kustahili                |
| 140. | <b>duress</b>               | lazimisha/shurutisha/tishia               |
| 141. | <b>duty</b>                 | wajibu/ ushuru                            |

## E

|      |                  |                         |
|------|------------------|-------------------------|
| 142. | <b>eligible</b>  | -enye sifa/inayostahili |
| 143. | <b>eliminate</b> | ondosha/futa/ teketeza  |
| 144. | <b>emolument</b> | malipo/ujira/ mshahara  |
| 145. | <b>enabling</b>  | kuwezesha               |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|      |                            |   |
|------|----------------------------|---|
| 146. | <b>enact/enacted</b>       | tunga (sheria)/imetungwa                            |
| 147. | <b>encumbrance</b>         | kizuizi/ adha                                       |
| 148. | <b>enforce</b>             | tekeleza/ lazimisha                                 |
| 149. | <b>endorse</b>             | thibitisha  |
| 150. | <b>enrol</b>               | sajili, andikisha                                   |
| 151. | <b>equity</b>              | hisa  |
| 152. | <b>equity/equitable</b>    | sawa/usawa/ haki                                    |
| 153. | <b>establish</b>           | anzisha/jenga hoja                                  |
| 154. | <b>estate</b>              | mali/ shamba/ eneo/ milki                           |
| 155. | <b>estop</b>               | zuia/ kataza  |
| 156. | <b>ethics</b>              | maadili   |
| 157. | <b>evade</b>               | kwepa   |
| 158. | <b>evict</b>               | ondoa/ fukuza                                       |
| 159. | <b><i>ex officio</i></b>   | kutokana na madaraka ya kiofisi au cheo/ isio rasmi |
| 160. | <b><i>ex parte</i></b>     | uamuzi/ mwenendo kwa upande mmoja                   |
| 161. | <b>examine/examination</b> | chunguza/uchunguzi/ uliza/ hoji/ mtihani            |
| 162. | <b>exclusive</b>           | -kipekee  |
| 163. | <b>execute</b>             | tekeleza  |
| 164. | <b>exempt/exemption</b>    | samehe/msamaha                                      |
| 165. | <b>expressly</b>           | wazi/dhahiri/bayana                                 |
| 166. | <b>extract</b>             | kidondoo/kiziduo                                    |

## F

|      |                             |   |
|------|-----------------------------|---|
| 167. | <b>facilitate</b>           | wezesha/ rahisisha  |
| 168. | <b>fee</b>                  | ada   |
| 169. | <b>fine</b>                 | faini   |
| 170. | <b>firm</b>                 | kampuni/shirika   |
| 171. | <b>foregoing</b>            | iliyotangulia/ iliyotajwa                                   |
| 172. | <b>foreign</b>              | -a kigeni/-a nje ya nchi / nje                              |
| 173. | <b>forfeit/forfeiture</b>   | twaa/utwaaji/ nyang'anya ( kwa adhabu ya kosa)/ poteza haki |
| 174. | <b>for the purpose/ for</b> | kwa madhumuni ya  |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|      |                    |   |
|------|--------------------|---|
|      | <b>purposes</b>    |   |
| 175. | <b>forthwith</b>   | haraka iwezekanavyo/ mara moja/ papo hapo |
| 176. | <b>forum</b>       | jukwaa/ baraza/ mkutano                   |
| 177. | <b>fund</b>        | mfuko/ fedha/ gharimia                    |
| 178. | <b>fundamental</b> | -a msingi/ asili                          |

### G

|      |                           |   |
|------|---------------------------|---|
| 179. | <b>gap</b>                | ombwe/ pengo/ upenyo/ umbali/ upungufu          |
| 180. | <b>Gazette</b>            | Gazeti la Serikali                              |
| 181. | <b>general provisions</b> | mashari ya jumla                                |
| 182. | <b>grant</b>              | toa/ridhaa/kubali/ mkopo wenyewe masharti nafuu |
| 183. | <b>gratuity</b>           | kiinua mgongo/ bahashishi                       |
| 184. | <b>grievance</b>          | malalamiko                                      |
| 185. | <b>grounds</b>            | sababu  |
| 186. | <b>guarantee</b>          | dhamana/ dhamini                                |

### H

|      |                              |  |
|------|------------------------------|--|
| 187. | <b>Hansard</b>               | kumbukumbu rasmi za mijadala ya Bunge/ Hansadi |
| 188. | <b>hearsay</b>               | uvumi/-a kusikia/ tetesi                       |
| 189. | <b>hereinafter contained</b> | kama yalivyoainishwa humo                      |
| 190. | <b>High Court</b>            | Mahakama Kuu                                   |
| 191. | <b>hinder</b>                | zuia/chelewesha                                |
| 192. | <b>holder</b>                | mmiliki / mwenye madaraka/ mshikiliaji wa muda |

### I

|      |                       |                              |
|------|-----------------------|------------------------------|
| 193. | <b>in addition to</b> | pamoja na/ nyongeza          |
| 194. | <b>in case of</b>     | ikitokea/ iwapo/ pale ambapo |
| 195. | <b>illegal</b>        | kinyume na sheria/ haramu    |

## ISTILAHII ZA KISHERIA

|      |                              |  |
|------|------------------------------|--|
| 196. | <b>immovable</b>             | isiyohamishika                                 |
| 197. | <b>immune</b>                | huru/isioweza kushtakiwa/-enye kinga           |
| 198. | <b>impartial</b>             | isiyopendelea/ adilifu/ -enye kufuata haki     |
| 199. | <b>implication</b>           | matokeo  |
| 200. | <b>imply</b>                 | maanisha/ husisha/ dokeza                      |
| 201. | <b>impose</b>                | toza/lazimisha / amuru/ toa ( adhabu, faini)   |
| 202. | <b>imprisonment</b>          | kifungo  |
| 203. | <i>in camera</i>             | faragha/ siri                                  |
| 204. | <b>incorporate</b>           | jumuisha/sajili kampuni                        |
| 205. | <b>indemnity/indemnify</b>   | malipo/lipia hasara/ fidia                     |
| 206. | <b>in accordance to</b>      | kwa mujibu wa                                  |
| 207. | <b>in accordance with</b>    | kulingana na                                   |
| 208. | <b>individual</b>            | mtu  |
| 209. | <b>in favour of</b>          | kwa manufaa ya                                 |
| 210. | <b>influence</b>             | shawishi/ushawishi/ ulevi                      |
| 211. | <b>infringe/infringement</b> | kiuka/ ukiukaji                                |
| 212. | <b>inquire/inquiry</b>       | chunguza/uchunguzi/ mahojiano                  |
| 213. | <b>injunction</b>            | zuio   |
| 214. | <i>in lieu</i>               | badala ya                                      |
| 215. | <b>in particular</b>         | hususan/mahususi/ maalumu/kwa namna ya kipekee |
| 216. | <b>in pursuance to</b>       | kwa kuzingatia                                 |
| 217. | <b>in relation</b>           | kuhusiana                                      |
| 218. | <b>in the course of</b>      | katika   |
| 219. | <b>in which case</b>         | katika hali hiyo                               |
| 220. | <b>insert</b>                | ingiza/weka                                    |
| 221. | <b>instalment</b>            | sehemu ya malipo/kulipa kidogo kidogo          |
| 222. | <b>instrument</b>            | hati/ hati rasmi                               |
| 223. | <b>intention</b>             | kusudi/ nia/ dhamira                           |
| 224. | <i>inter partes</i>          | uamuzi/ mwenendo wa pande zote                 |
| 225. | <i>inter alia</i>            | pamoja na mambo mengine                        |
| 226. | <b>interest</b>              | maslahi/ wiwa/ riba                            |
| 227. | <b>interfere</b>             | ingilia kati                                   |

## ISTILAHIZA KISHERIA

|      |   |                                    |
|------|---|------------------------------------|
| 228. | <b>interpret/interpretation / translation</b> | fasiri/tafsiri/ fafanua/ ukalimani |
| 229. | <b>intervene</b>                              | ingilia kati                       |
| 230. | <b>irregularity</b>                           | kasoro/hitilafu/ upungufu          |
| 231. | <b>issue</b>                                  | suala/jambo/ mtoto                 |

### J

|      |                        |   |
|------|------------------------|---|
| 232. | <b>joint venture</b>   | ubia  |
| 233. | <b>judgement</b>       | Hukumu                                      |
| 234. | <b>judicial notice</b> | utambuzi bila ushahidi/utambuzi wa mahakama |
| 235. | <b>jurisdiction</b>    | mamlaka/ mipaka ya kisheria/                |
| 236. | <b>justice</b>         | haki  |

### L

|      |                         |   |
|------|-------------------------|---|
| 237. | <b>labour relations</b> | uhusiano kazini   |
| 238. | <b>lapse</b>            | kuisha/ kupita muda   |
| 239. | <b>legal action</b>     | hatua za kisheria   |
| 240. | <b>legislation</b>      | sheria  |
| 241. | <b>liable</b>           | wajibika  |
| 242. | <b>limit</b>            | mpaka/ukomo/ zuia   |
| 243. | <b>local content</b>    | ushirikishaji wazawa  |
| 244. | <b>locus standi</b>     | haki ya kuanzisha shauri / kuwa na sifa ya kuanzisha madai mbele ya mahakama au chombo chochote cha utoaji haki |

### M

|      |                             |                                     |
|------|-----------------------------|-------------------------------------|
| 245. | <b>maintain/maintenance</b> | tunza/dumisha/endeleza/matunzo      |
| 246. | <b>mandate</b>              | mamlaka/ uwezo                      |
| 247. | <b>material</b>             | ya muhimu/-enyе maana/msingi/ vifaa |
| 248. | <b>matter</b>               | suala/jambo/hoja                    |
| 249. | <b>Memorandum of</b>        | hati ya makubaliano/ hati ya        |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|      |                                  |                                       |
|------|----------------------------------|---------------------------------------|
|      | <b>understanding</b>             | maridhiano                            |
| 250. | <b>memorandum of association</b> | katiba ya kampuni                     |
| 251. | <b>merit</b>                     | -enye kustahili/ sifa/ msingi         |
| 252. | <b>mischief</b>                  | madhara/ changamoto/hasara            |
| 253. | <b>misconduct</b>                | mwenendo mbaya                        |
| 254. | <b>miscellaneous provisions</b>  | masharti mengineyo                    |
| 255. | <b>misinterpretation</b>         | tafsiri isiyo sahihi                  |
| 256. | <b>misuse</b>                    | tumia vibaya/ matumizi mabaya         |
| 257. | <b>money/monies</b>              | fedha                                 |
| 258. | <b>morals</b>                    | maadili                               |
| 259. | <b>mortgage</b>                  | rehani/ dhamana/ kuweka poni          |
| 260. | <b>mutatis mutandis</b>          | pamoja na mabadiliko muhimu yanayofaa |
| 261. | <b>mutual</b>                    | iliyokubalika na pande mbili au zaidi |

## N

|      |                        |                         |
|------|------------------------|-------------------------|
| 262. | <b>native</b>          | mzawa/mwenyeji          |
| 263. | <b>necessary</b>       | muhimu/-a lazima        |
| 264. | <b>negative</b>        | hasi                    |
| 265. | <b>negotiation</b>     | majadiliano             |
| 266. | <b>nominate</b>        | pendekeza               |
| 267. | <b>non appearance</b>  | shindwa kufika/kutofika |
| 268. | <b>notary public</b>   | mthibitishaji wa umma   |
| 269. | <b>notice</b>          | notisi                  |
| 270. | <b>notwithstanding</b> | bila kujali             |
| 271. | <b>null</b>            | batili                  |

## O

|      |                         |                         |
|------|-------------------------|-------------------------|
| 272. | <b>oath</b>             | kiapo                   |
| 273. | <b>object/objective</b> | lengo/kusudio/madhumuni |
| 274. | <b>obligation</b>       | wajibu                  |
| 275. | <b>obstruct</b>         | zuia/ kinga             |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|      |                                    |   |
|------|------------------------------------|---|
| 276. | <b>occupy/occupation/ occupant</b> | miliki/umiliki/mmiliki/kaa/ukaaji/mka aji/ kazi |
| 277. | <b>offence</b>                     | kosa  |
| 278. | <b>offer</b>                       | ofa/toa ahadi/weka dau                          |
| 279. | <b>omit</b>                        | ondoa/acha                                      |
| 280. | <b>opt</b>                         | chagua/amua                                     |
| 281. | <b>order</b>                       | amri/agiza                                      |
| 282. | <b>ordinance</b>                   | sheria/ sheria kabla ya uhuru                   |
| 283. | <b>organ</b>                       | chombo/ kiungo                                  |
| 284. | <b>organize</b>                    | panga/weka sawa/ andaa                          |
| 285. | <b>organisation</b>                | shirika/asasi/mpangilio                         |
| 286. | <b>own/ownership</b>               | miliki/umiliki                                  |

### P

|      |                               |   |
|------|-------------------------------|---|
| 287. | <b>paragraph/subparagraph</b> | aya/aya ndogo/para  |
| 288. | <b>proclamation</b>           | tamko/ tamko maalumu  |
| 289. | <b>partner</b>                | mshirika/mbia   |
| 290. | <b>penal code</b>             | kanuni za adhabu  |
| 291. | <b>pending</b>                | inayoendelea/inayongoja uamuzi  |
| 292. | <b>perform</b>                | tenda/tekeleza  |
| 293. | <b>permit</b>                 | kibali/ruhusa/ ruhusu   |
| 294. | <b>perpetual succession</b>   | mwendelezo wa kurithi/ dumisha  |
| 295. | <b>petition</b>               | maombi  |
| 296. | <b>power</b>                  | mamlaka/madaraka/uwezo/ nishati   |
| 297. | <b>power of attorney</b>      | mamlaka ya kisheria ya kumwakilisha mtu/ hati ya uwakilishi ya kisheria |
| 298. | <b>practice</b>               | desturi/tekeleza shughuli/ taratibu                                     |
| 299. | <b>preamble</b>               | utangulizi/ dibaji  |
| 300. | <b>precede</b>                | -a kutangulia   |
| 301. | <b>preclude</b>               | zuia/kataza   |
| 302. | <b>predetermine</b>           | iliyopangwa awali   |
| 303. | <b>prefer</b>                 | pendelea/bora zaidi   |
| 304. | <b>preliminary</b>            | mwanzo/utangulizi   |
| 305. | <b>prescribe</b>              | ainisha/ eleza/ fafanua   |

## ISTILAHIZA KISHERIA

|      |                                |   |
|------|--------------------------------|---|
| 306. | <b>presume/presumption</b>     | kisia/dhania/chukulia/ dhana            |
| 307. | <b>prevail</b>                 | tawala/ tumika/ shinda                  |
| 308. | <b>prevent</b>                 | zuia/ kataza                            |
| 309. | <b><i>prima facie</i></b>      | ushahidi uliojitosheleza/ dhahiri       |
| 310. | <b>principal</b>               | mkuu/ kuu                               |
| 311. | <b>prior</b>                   | kabla/ awali                            |
| 312. | <b>provided for</b>            | iliyoainishwa                           |
| 313. | <b>provided that</b>           | isipokuwa kwamba                        |
| 314. | <b>privilege</b>               | upendeleo/ haki/ stahiki                |
| 315. | <b>procedure</b>               | utaratibu                               |
| 316. | <b>proceed</b>                 | endelea                                 |
| 317. | <b>proceeds</b>                | mapato yatokanayo                       |
| 318. | <b>proceedings</b>             | mwenendo                                |
| 319. | <b>produce</b>                 | zalisha/ toa/ wasilisha/ zao/ tengeneza |
| 320. | <b>profession/professional</b> | taaluma/utaalamu/mtaalamu               |
| 321. | <b>prohibit</b>                | zuia/ kataza                            |
| 322. | <b>proof/prove</b>             | uthibitisho/thibitisha                  |
| 323. | <b>propose</b>                 | pendekeza                               |
| 324. | <b>proviso</b>                 | kivuo                                   |
| 325. | <b>public</b>                  | umma/hadhira/hadhara                    |
| 326. | <b>punishment</b>              | adhabu                                  |

## Q

|      |                              |                                     |
|------|------------------------------|-------------------------------------|
| 327. | <b>qualify/qualification</b> | kuwa na sifa/sifa                   |
| 328. | <b>quorum</b>                | akidi                               |
| 329. | <b>quasi judicial body</b>   | chombo chenye mamlaka ya kimahakama |

## R

|      |                             |  |
|------|-----------------------------|--|
| 330. | <b>rate</b>                 | kima/kiwango/ kodi/bei / tathmini/<br>kadiria          |
| 331. | <b>ratify/ ratification</b> | ridhia/idhinisha/ thibitisha/ uthibitisho<br>(mkataba) |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|      |  |   |
|------|--|---|
| 332. | <b>receipt</b>                         | stakabadhi/ risiti/kupokea  |
| 333. | <b>reciprocal</b>                      | kukubaliana/ kupeana/ kubadilishana/ kuhusiana/ kutendeana (kwa pande mbili ) |
| 334. | <b>recognise/recognition</b>           | tambua/utambuzi   |
| 335. | <b>recommend</b>                       | pendekeza/ shauri   |
| 336. | <b>reconcile/reconciliation</b>        | patana/mapatano   |
| 337. | <b>rectify/rectification</b>           | sahihisha/masahihisho   |
| 338. | <b>refer</b>                           | rejea/ peleka   |
| 339. | <b>reference</b>                       | marejeo/marejeleo/kumbukumbu  |
| 340. | <b>register/registration/registrar</b> | sajili/rejestra/ daftari/usajili/msajili                                      |
| 341. | <b>registry</b>                        | masijala  |
| 342. | <b>regulate/regulation</b>             | dhibiti/simamia/udhibiti/usimamizi  |
| 343. | <b>regulations</b>                     | kanuni  |
| 344. | <b>relief</b>                          | nafuu/ msaada (Mfuko wa msaada)   |
| 345. | <b>remedy</b>                          | nafuu/ tiba/ rekebisha  |
| 346. | <b>remission</b>                       | msamaha   |
| 347. | <b>remit</b>                           | samehe/ondolea/futa/ achilia  |
| 348. | <b>renew</b>                           | fanya upya tena/ ongeza muda/ huisha  |
| 349. | <b>repeal</b>                          | futa/ batilisha/tengua/ tangua  |
| 350. | <b>replace</b>                         | badilisha/weka badala ya/ rudisha mahali pake                                 |
| 351. | <b>require/requirement</b>             | taka/hitaji/takwa/ sharti   |
| 352. | <b>reserve</b>                         | hifadhi/weka<br>akiba,nafasi/tenga/bakiza                                     |
| 353. | <b>reservation</b>                     | sita/tilia shaka/ bakiza  |
| 354. | <b>residence/resident</b>              | makazi/ makao/maskani/ mkazi  |
| 355. | <b>resign</b>                          | jiuzulu/ng'atuka/ jitoa/ acha kazi/ jiengua                                   |
| 356. | <b>resolution</b>                      | azimio/uamuzi   |
| 357. | <b>respectively</b>                    | mtawalia  |
| 358. | <b>responsible/responsibility</b>      | wajibika/husika/wajibu/jukumu/dhima /madaraka                                 |
| 359. | <b>restrain</b>                        | zuia/ katazo/ nyima/ rudisha/ dhibiti   |
| 360. | <b>restrict</b>                        | wekea mipaka/zuia/kataza/bana/dhibiti   |

## ISTILAHIA ZA KISHERIA

|      |                           |   |
|------|---------------------------|---|
| 361. | <b>review</b>             | marejeo/pitia/tafakari upya/angalia<br>upya/hakiki        |
| 362. | <b>revision</b>           | mapitio/masahihisho                                       |
| 363. | <b>revoke/ revocation</b> | batalisha/futa/tangua/utenguaji                           |
| 364. | <b>right</b>              | haki/sahihi/kweli/sawa/halisi/upande<br>wa kuume au kulia |
| 365. | <b>royalty</b>            | mrabaha   |
| 366. | <b>rule</b>               | amri/sharti/kanuni/<br>desturi/amuru/tawala               |
| 367. | <b>rules</b>              | kanuni  |
| 368. | <b>ruling</b>             | uamuzi/uamuzi mdogo/-a kutawala<br>(utawala wa machifu)   |
|      |                           |   |

### S

|      |                             |   |
|------|-----------------------------|---|
| 369. | <b>sample</b>               | sampuli/kielelezo   |
| 370. | <b>sanction</b>             | idhini/ruhusa/kibali/kikwazo au<br>vikwazo                |
| 371. | <b>satisfy/satisfaction</b> | tosheleza/ridhisha/kidhi/kuridhisha                       |
| 372. | <b>save for</b>             | isipokuwa kwa   |
| 373. | <b>savings provisions</b>   | masharti ya mwendelezo                                    |
| 374. | <b>schedule</b>             | jedwali   |
| 375. | <b>scheme</b>               | mpango/mpangilio/mradi                                    |
| 376. | <b>scope</b>                | wigo/mawanda  |
| 377. | <b>scrutinise/scrutiny</b>  | chunguza/pekuwa/uchunguzi/upekuzi                         |
| 378. | <b>seal</b>                 | lakiri/muhuri/chapa                                       |
| 379. | <b>section/subsection</b>   | kifungu/kifungu kidogo/sehemu                             |
| 380. | <b>seize/ seizure</b>       | shika/kamata/nyanga'anya/twaa/ukam<br>ataji               |
| 381. | <b>service</b>              | utumishi/huduma/kuwasilisha                               |
| 382. | <b>short title</b>          | jina fupi   |
| 383. | <b>society</b>              | chama/shirika/jamii/umoja                                 |
| 384. | <b>specific</b>             | mahuususi   |
| 385. | <b>specified</b>            | iliyoainishwa/ iliyotajwa/ iliyoelezwa/<br>iliyobainishwa |

## ISTILAHIZA KISHERIA

|      |                               |   |
|------|-------------------------------|---|
| 386. | <b>status</b>                 | hadhi/hali/cheo                                 |
| 387. | <b><i>Status quo</i></b>      | hali kama ilivyo                                |
| 388. | <b>stipulate</b>              | ainisha/tamka/weka masharti                     |
| 389. | <b>subject to</b>             | kwa kuzingatia                                  |
| 390. | <b>submit</b>                 | wasilisha/salimisha/kabidhi/tii                 |
| 391. | <b>subordinate</b>            | -a chini/saidizi                                |
| 392. | <b>substantive</b>            | -a msingi/halisi                                |
| 393. | <b>substitution</b>           | badala/mbadala                                  |
| 394. | <b>suit</b>                   | shauri la madai                                 |
| 395. | <b>summary (summary suit)</b> | mashauri yasiyofuata utaratibu wa kawaida       |
| 396. | <b>summons</b>                | samansi/wito wa mahakama au chombo cha kisheria |
| 397. | <b>suspend</b>                | ahirisha/sitisha/zuia kwa muda                  |

## T

|      |                                |   |
|------|--------------------------------|---|
| 398. | <b>tax</b>                     | kodi/ushuru                                   |
| 399. | <b>technicalities</b>          | -a kiufundi/-a kitaalamu                      |
| 400. | <b>tender</b>                  | tenda/zabuni/wasilisha/kabidhi/uchanga/-ororo |
| 401. | <b>tenure</b>                  | kipindi/muda wa kushika ofisi                 |
| 402. | <b>term</b>                    | muhula/muda/kipindi/masharti                  |
| 403. | <b>transitional provisions</b> | masharti ya mpito                             |
| 404. | <b>treasury bill</b>           | hatifungani                                   |
| 405. | <b>title deed</b>              | hatimiliki                                    |
| 406. | <b>trial</b>                   | usikilizaji wa shauri au shtaka/daawa/jaribio |
| 407. | <b>tribunal</b>                | baraza  |
| 408. | <b>trust/trustee</b>           | amana/mdhamini/amini                          |

## U

|      |                 |   |
|------|-----------------|---|
| 409. | <b>unfair</b>   | isiyo sawa/-enye upendeleo/-enye uonevu |
| 410. | <b>unlawful</b> | isiyo halali/kinyume na sheria          |

## ISTILAHI ZA KISHERIA

### V

|      |                            |  |
|------|----------------------------|--|
| 411. | <b>valid</b>               | msingi/halali/kweli/thabiti                  |
| 412. | <b>vary</b>                | badili/geuza/badilisha                       |
| 413. | <b>verify/verification</b> | thibitisha/uthibitisho/hakikisha/dhihiri sha |
| 414. | <b>vest</b>                | toa madaraka kisheria/kabidhi                |
| 415. | <b>vet/vetting</b>         | hakiki/kagua/pekuwa/uhakiki/ukaguzi/u pekuzi |
| 416. | <b>veto</b>                | kura ya turufu                               |
| 417. | <b>void</b>                | batili                                       |

### W

|      |                          |  |
|------|--------------------------|--|
| 418. | <b>waive</b>             | samehe   |
| 419. | <b>warrant</b>           | waranti/hati ya idhini ya kutenda jambo/kibali |
| 420. | <b>when</b>              | pale ambapo                                    |
| 421. | <b>where</b>             | endapo/iwapo                                   |
| 422. | <b>whereas</b>           | kwa kuwa                                       |
| 423. | <b>withdraw</b>          | ondoa/futa/toa                                 |
| 424. | <b>withhold</b>          | zuia/shikilia                                  |
| 425. | <b>without prejudice</b> | bila kuathiri                                  |
| 426. | <b>written law</b>       | sheria/sheria ndogo                            |

### Z

|      |             |                 |
|------|-------------|-----------------|
| 427. | <b>zone</b> | zoni/eneo/kanda |
|------|-------------|-----------------|

**ZIMETAYARISHWA NA:**  
**Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali**  
**Mji wa Serikali - Mtumba**  
**S.L.P 630, DODOMA**  
**TANZANIA**

Haki zote zimehifadhiwa ©2023